# TANESCO MTANDAONI

Jarida la Mtandaoni | Mei 22, 2024







# TANESCO INAVYOUTEKELEZA MKAKATI WA USHIRIKISHAJI WADAU NCHINI

- Ni kwa kuwezesha ofisi za mikoa na wilaya kuwafikia wadau
- Wadau kufahamu maendeleo ya miradi ya umeme inayotekelezwa
- Viongozi wa serikali wasema itasaidia kupunguza maswali kwa wananchi
- Mikoa ya Iringa, Kilimanjaro, Simiyu, Mwanza, Shinyanga yaanza utekelezaji



# KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI YAPONGEZA KASI YA UJENZI WA MRADI WA KITUO CHA KUPOZA UMEME CHALINZE

**Na. MayLoyce Mpombo, Chalinze**

Kamati ya kudumu ya bunge ya Nishati na Madini imeipongeza serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa utekelezaji wa mradi wa kituo cha kupoza umeme pamoja na mradi wa njia ya kusafirishia umeme kutoka JNHPP hadi Chalinze.

Akizungumza mara baada ya kutembelea kituo hiko Mei 18, 2024 Chalinze Mkoa wa Pwani Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Kirumbe Ng'enda amesema ni kazi kubwa imefanyika katika kituo hiko ikiwa ni katika kipindi kifupi cha uongozi wa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan.

> Tulikuja hapa mwezi wa tatu kuangalia maendeleo ya kituo hiki na kilikuwa kimefika asilimia 55 na tulipata wasiwasi na kuwaomba waongeze spidi kwa maana Bwawa la Mwalimu Nyerere lilikuwa kwenye kasi kubwa na leo tumejionea kutoka asilimia 55 mpaka kufikia asilimia 93.5 kazi kubwa imefanyika tunawapongeza sana serikali kupitia wizara hii ya nishati
>
> - Mhe. Ng'enda

Amesema kukamilika kwa mradi huu utachochea sera ya nchi ya uchumi wa viwanda kwa kuwa hakuna maendeleo ya viwanda pasipokuwa na nishati ya umeme.



Aidha, ameongeza kukamilika kwa mradi huu pia unaenda kuondoa changamoto ya upungufu wa umeme lakini pia ukizidi utaweza kuuzwa kwa nchi jirani na hivyo kuchochea uchumi wa nchi kuzidi kukua.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Kapinga amesema miradi hiyo ambayo ipo ukingoni kukamilika ilianza mwaka 2021 chini ya serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dkt Samia Suluhu Hassan.

> Tunapomaliza miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dkt Samia tunayo miradi ya kujivunia njia ya kusafirishia umeme na kituo cha kupoza umeme yote ilianza 2021 ni miradi ambayo ilianza na awamu ya sita ambapo mradi wa njia ya kusafirishia umeme umefikia asilimia 99.5 na kituo cha kupoza umeme umefikia asilimia 93.7 miradi inatekelezeka na ipo mbioni kukamilika
>
> **- Mhe. Kapinga**

Pia ameipongeza TANESCO kwa usimamizi mzuri miradi hiyo ambayo imekuwa na tija na maslahi mapana kwa Taifa.

Akizungumzia swala la upatikanaji wa umeme nchini amesema umeme upo wa kutosha na nchi imeanza kunufaika kutokana na bwawa la Julius Nyerere ambapo megawati 235 za mashine namba 9 kutoka Bwawa la JNHPP zinapitishwa kwenda kwenye kituo cha kupoza umeme Chalinze.

Amesema ukatikaji wa umeme kwenye baadhi ya maeneo hausababishi na ukosefu wa nishati hiyo bali unatokana na uchakavu wa miundombinu ya kusafirishia umeme.

> Miundombinu kwenye baadhi ya maeneo ni chakavu na ya siku nyingi hivyo tunaendelea kufanyia kazi wakati kwa wakati ili kuboresha na watu wapate uhakika wa umeme wakati wote
>
> **- Mhe. Kapinga**

Naye, Meneja wa kituo cha kupoza umeme Mha. Newton Mwakifwamba amesema utekelezaji wa mradi kituo cha kupoza umeme umefikia asilimia 93.7 huku ujenzi wa njia ya kusafirishia umeme kutoka JNHPP hadi Chalinze ukiwa umefikia asilimia 99.5 wakati ujenzi kituo cha kuendeshea mitambo kikiwa kimekamilika kwa asilimia 100.

Ameongeza mpaka sasa mradi huo umefanikiwa kusafirisha Megawati 235 kutoka bwawa la JNHPP kwenda Chalinze na kuziingiza kwe gridi ya Taifa

> **Miradi hii imewezesha kukamilika kwa miundombinu wezeshi ya kupokea umeme zaidi na kuingiza kwenye Gridi ya Taifa ambapo umeme huu umefanikiwa kumaliza mgao wa umeme**
>
> **- Mha. Mwakifwamba.**

Mradi wa huu umegharimu kiasi cha shilingi bilioni 158 kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirishia umeme na shilingi Bilioni 128 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kupoza umeme chalinze ambapo miradi hiyo ilianza 2021.

## MATUKIO KATIKA PICHA



*Mhandisi **Newton Mwakifwamba** akiongoza ugeni wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Nishati na Madini katika maeneo ya mradi wa kituo cha kupoza umeme Chalinze katika ziara ya kukagua maendeleo ya mradi huo.*



*Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Judith Salvio Kapinga akizungumza mbele ya Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini katika kikao kazi cha maendeleo ya mradi wa kupoza umeme Chalinze mkoani Pwani Jumamosi Mei 18, 2024*



# DC - KHERI JAMES AWAASA WAKANDARASI UMEME IRINGA KUZINGATIA WELEDI

**Na. Augustino Kasale, Iringa**

Mkuu wa Wilaya ya Iringa Komred Kheri James amewataka wakandarasi wenye leseni za umeme Mkoani Iringa kufanya kazi kwa weledi katika kazi zao.

Ameyasema hayo tarehe 17 Mei 2024 Mkoani Iringa wakati wa kufungua kikao kilicholikutanisha Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Iringa na wakandarasi wenye leseni za umeme Mkoani Iringa, kilichokuwa na lengo la kujadili mikakati ya kuboresha huduma kwa mteja.

> Wakandarasi wa umeme ni vyema mkazingatia weledi wakati mnatekeleza majukumu yenu ili kuhakikisha mteja anapata huduma yenye viwango
>
> **- Komred Kheri James**

Ameongeza kuwa ubora wa kazi wanazofanya wakandarasi ni muhimu kwani hujenga sifa nzuri ya TANESCO na wakandarasi kwa mteja, huku akisisitiza kutoruhusu vishoka (watu wasio waaminifu) kuingilia fani yao kwani inaharibu taswira ya kazi yao kwa wateja.




> Pia , wananchi wengi hawana vipato vikubwa hivyo gharama za kuweka mtandao wa nyaya kwenye nyumba (waring) mnazowatoza jitahidini ziwe na unafuu ilikuwasadia kumudu gharama hizo
>
> **- Komred Kheri James**

Komred Kheri James ameeleza kuwa Serikali imejipanga kuhakikisha inazalisha umeme wa kutosha, na inakamilisha kazi ya usambazaji wa umeme.

Akizunguzia Wilaya ya Iringa, Komred Kheri James ameeleza kuwa Serikali imekamilisha zoezi la kusambaza umeme katika vijiji vyote na sasa imetenga kiasi cha shilingi bilioni 26 ili kwenda kuanza hatua ya vitongoji.

Nae, Kaimu Meneja wa Mkoa wa Iringa Mhandisi Herman Bucheye amesema kuwa kukutana na wakandarasi wenye leseni za umeme mkoani humo ni kuwakumbusha wajibu wao, kupokea maoni na kujibu hoja zao ili kuhakikisha mteja anapata huduma nzuri.



Wakizungumza mara baada ya kukamilika kwa kikao hicho, wakandarasi wameipongeza TANESCO na wameahidi kuongeza weledi na kushirikiana na TANESCO.




# TANESCO SIMIYU YAELEZA MIKAKATI YAKE KWA WADAU

**Na Shamu Lameck, Simiyu**

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Simiyu limesema kuwa tayari Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 97 kwa ajili ya kutekeleza miradi miwili mikubwa ya umeme itakayosaidia kutatua kero ya mara kwa mara ya kukatika kwa umeme katika mkoa huo.

Miradi hiyo ni pamoja na kituo cha kupozea umeme ambacho kinajengwa katika eneo la Imalilo Mjini Bariadi pamoja na ujenzi wa njia kubwa kusafirisha umeme wa msongo wa kilovolti 220 Kutoka Ibadakuli Mkoani Shinyanga hadi Imalilo Mkoani Simiyu

Hayo yamebainishwa tarehe 16 Mei 2024 na Meneja wa TANESCO Simiyu Mha. Alistidia Clemence wakati wa mkutano wa wadau, ambao ulilenga kuwashirikisha kwenye miradi inayotekelezwa na Shirika hilo mkoani humo.

Amesema kuwa mradi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Ibadakuli hadi Imalilo utekelezaji wake umefikia asilimia 35 na unagharimua kiasi cha Shilingi Bilioni 48 huku mradi wa kituo cha kupozea umeme ukigharimu Shilingi Bilioni 49.

> Leo tumeona tuwaite wadau wetu ambao ni wateja wa TANESCO kuwaeleza juu ya utekelezaji wa mradi huu na kuwatambulisha wakandarasi wanaotekeleza mradi huo, umekuwa mradi wa muda mrefu lakini leo tumekuja kuwaeleza kuwa tayari serikali imetoa fedha za kutekeleza mradi huu
>
> **- Mhe. Alistidia**

Kwa upande wake, Msimamizi wa Mradi huo Mhandisi Adolfu Kigombola, amewahakikishia wananchi wa Mkoa huo kuwa miradi yote miwili itatekelezwa ndani ya muda uliopangwa na wataondoakana na adha ya kukatika katika kwa umeme kila wakati.

> Tumekubaliana na mkandarasi wa kituo cha kupokea na kupoza umeme kikamilike kufikia mwezi juni 2025 kama ilivyo kwenye mkataba wake
>
> **- Mha. Adolfu Kigombola**

Aidha wakati wa ufunguzi wa kikao hicho Mkuu wa Mkoa Simiyu Mhe. Dkt. Yahaya Nawanda amesema kuwa, Serikali imekuwa ikitenga fedha nyingi kwa ajili ya Mkoa wa Simiyu



> Mwaka huu kwenye fedha zaidi ya trioni 1.4 kati yake bilioni 177 zimetengwa kwa ajili ya umeme
>
> **- Mhe. Dkt. Yahaya Nawanda**

Mhe. Nawanda amesema kiwango cha fedha kilichotengwa kina ashiria dhamira ya kweli ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kumaliza kero ya umeme.



# TANZANIA KUNUFAIKA NA UANACHAMA WA JUMUIYA ZA NISHATI ZA UKANDA WA AFRIKA MASHARIKI (EAPP) NA NCHI ZILIZO KUSINI MWA AFRIKA (SAPP)

**Na Charles Kombe, Dar es Salaam**

Tanzania inatarajiwa kunufaika na uanachama wake katika jumuiya za nishati za Afrika Mashariki yaani (East African Power Pool) na Kusini (South Africa Power Pool) katika maeneo mbalimbali ikiwemo biashara ya umeme pamoja na kuunganishwa katika gridi ya pamoja.

Hayo yamebainishwa tarehe 13 Mei 2024 katika warsha ya siku tano iliyowakutanisha wakuu wa sekta ya nishati pamoja na washauri kutoka nchi 13 Afrika katika Hoteli ya Ramada wanaokutana kujadili na kupanga mikakati mbalimbali ya namna ya kuunda kanuni za soko la nishati ya umeme (Market rules) katika biashara ya kuuziana umeme kwenye kanda hizo.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji kutoka TANESCO wakiwa ni Shirika mwenyeji linalotoa huduma ya umeme nchini Naibu Mkurugenzi mtendaji usafirishaji umeme Mhandisi Abubakar Issa amesema Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya za nishati za ukanda wa Afrika Mashariki (EAPP) na kusini mwa Afrika (SAPP) ambazo lengo lake ni kuwezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika nchi hizo kwa kuangalia biashara ya kuuziana umeme na uwepo wa gridi ya pamoja.

> Sisi kama Tanzania tutakuwa na uwezo wa kuuza au kununua umeme katika jumuiya za nishati za Afrika Mashariki na Kusini. Kitendo cha miundombinu yetu itakapokuwa imeunganisha jumuiya zote mbili, tutafaidika na mapato kama nchi. Na hii pia itasaidia kuhakikisha nchi zote za Afrika zinasaidiana katika kuwa na umeme wa uhakika. Hili litakuza uchumi wa Tanzania pamoja na bara letu kwa ujumla kwa kuwa umeme ni uchumi
>
> **- Mha. Issa**

Amesema hadi sasa miundombinu inaendelea kuunganishwa na malengo ni kwamba biashara ianze mara tu muunganiko wa miundombinu hiyo itakapokamilika.

> Tunaunganisha ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika mfano sisi na Kenya tayari na kwa sasa tunaendelea na Zambia ambapo kwa upande wake, Tanzania tuko tayari na tutakuwa tayari zaidi pale miundombinu inayoendelea kujengwa itakapokamilika
>
> **- Mha. Issa**

Aliongeza kuwa kwa sasa Tanzania imeanza kwa kuunganisha nchi za Kusini na Mashariki kisha Kanda za Magharibi na Kaskazini zitakuwa tayari na baadae kuwa na muunganisho wa gridi Afrika nzima ili nchi zote ziweze kuuziana umeme.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Nishati ya Afrika Mashariki EAPP, James Wahogo, amesema wanatazama namna Mashirika hayo ya umeme yatatumia kanuni za soko zitakazoafikiwa katika warsha hiyo.

> Baada ya kujadili katika warsha hii zitapelekwa baraza la Mawaziri wa Nishati katika nchi hizi ambao wana mamlaka ya kuzipitisha ili ziwe sheria kamili. Hadi 2027 tunategemea Jumuiya ya Mashariki na Kusini zitakuwa tayari zimeshakamilika ambapo wananchi watafaidika kwa kuwa watakuwa watapata umeme kwa bei nafuu
>
> **- Wahongo**

Naye, Crispen Zana kutoka Shirika la Maendeleo Afrika AUDA NEPAD yenye lengo la kuwa na gridi inayounganisha nchi zote za Afrika amesema kuna Waafrika takribani milioni 600 wanaishi gizani hivyo faida ya jambo hili ni kuhakikisha upatikanaji umeme unawezekana kwa Waafrika wote.

> Nchi moja ikizalisha umeme mkubwa itauzia nyingine na hii ndivyo itakavyokuwa. Lazima tuangalie mikakati ya kuwasaidia wananchi wetu katika miaka zaidi ya 10 ijayo. Jitihada za kila nchi ni kuwa na umeme ambao unatumiwa na watu pamoja na uchumi kwa ujumla
>
> - Zana

Kuanzishwa kwa sheria za kuongoza soko la umeme kunatarajiwa kuimarisha hali ya upatikanaji umeme nchini kwa ubadilishanaji wa umeme unaovuka mipaka na kuimarisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Kupitia kusanyiko hili Washiriki walibadilishana maarifa na uzoefu na kufanya maamuzi ya pamoja ili kuunda sheria thabiti za soko zinazolenga kuongoza sekta ya nishati ya Afrika Mashariki.

Warsha hiyo ya siku tano inayoendelea inakutanisha wadau kutoka nchi wanachama za Tanzania, Kenya, Uganda, Misri, Ethiopia, Libya, Rwanda, Burundi, Sudan Kusini, Sudan, Djibouti, Somalia pamoja na Congo DRC.

## MATUKIO KATIKA PICHA







## HABARI KWA UFUPI

# TANESCO YASHIRIKI MKUTANO WA WADAU WAKE MWANZA NA KUTATUA CHANGAMOTO ZA WATEJA WAKE ILEMELA

**Na. Prisca Kayanga, Ilemela - Mwanza**

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoa wa Mwanza limeshiriki mkutano wa kusikiliza na kutatua kero za wananchi ulioandaliwa na Mkuu wa Wilaya ya Ilemela Mhe. Hassan Masala katika kata ya Kirumba mtaa wa Kiloleli ambapo eneo hilo lilikuwa na mgogoro wa ardhi ambayo laini ya umeme ilipita katika kiwanja cha Bw. Nasib Rajab Ismail

Katika kutatua kero hizo, Mkuu wa Wilaya amewaagiza Tanesco

- Kuendelea kufata taratibu za kushirikiana na serikali ya mtaa pale wanapotaka kujenga laini ya umeme.
- Kuendelea kutatua kero mbali mbali za wateja kwa wakati.
- Kuhakikisha kuwa wanasimamia kanuni na taratibu husika pindi mteja anapounganishiwa huduma ya umeme



Pia alitumia nafasi hiyo kuipongeza TANESCO kwa kuzidi kuimarisha hali ya upatikanaji wa Umeme katika wilaya hiyo huku akizidi kuwasisitiza kwamba hali hiyo iendelee kwa mustakabali mzuri wa wilaya ya Ilemela



Pamoja na hayo, Idara ya Uhusiano na huduma kwa wateja ilipata fursa ya kutembelea wateja wa maeneo ya Luchelele nyumba kwa nyumba wanaopokea umeme kutoka kwenye Mashine umba ya Michungwani kuwataarifu zoezi la kuhamisha laini ya umeme kupisha ujenzi wa barabara, litakalopelekea kukosekana kwa huduma ya umeme kwa muda wa masaa nane (8) ambapo zoezi hilo lilipongezwa na wakazi wa Luchelele na kufurahishwa na maboresho hayo ya huduma kwa wateja




# TANESCO KILIMANJARO NA WADAU CLINIC

**Na. Mwanaisha Mbita, Moshi**

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Kilimanjaro kwa kushirikiana na Jeshi la zimamoto na uokoaji Mkoa wa Kilimanjaro wametoa elimu kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Moshi pamoja na kiwanda cha Serengeti namna ya kujikinga na majanga ya moto kwenye maeneo yao ikiwemo kazini na majumbani lakini pia:-

- Elimu ya "Power factor" kwa Viwanda
- Matumizi sahihi ya Umeme
- Matumizi ya "AMR system" kwa wateja wenye mita hizo
- Ulinzi wa miundombinu ya Umeme
- Elimu ya usalama
- Uelewa juu ya njia za mawasiliano

Hayo yamefanyika Siku ya Mei 13, 2024 ambapo Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Elias Manyama wa kitengo cha elimu kwa umma udhibiti wa majanga ya moto mkoa wa Kilimanjaro ameleza sababu ya kutoa elimu hiyo ni kuelimisha namna gani ya kujikinga na majanga ya moto na matumzi sahihi ya Nishati ya Umeme nakujua hatua gani za kufanya wakati wa matukio ya moto.



Kwa upande wake, Mchungaji Jones Mola Askofu Mkuu wa Kanisa la Amani Tanzania amelipongeza Shirika la Umeme nchini Tanesco na Serikali kwa kazi kubwa wanayofanya ya kutoa huduma ya Umeme na elimu kwa watumiaji wa Umeme hali itakayo saidia kupungaza majanga ya moto katika maeneo mbalimbali na kusaidia usalama mahala pakazi.

Afisa Uhusino wa TANESCO Mkoa wa Kilimanairo, Aisha Mbita ameeleza lengo la kuleta huduma hii ya wadau clinic ni kuwapa elimu Viongozi, Mashirika, Kampuni na wadau muhimu wa Shirika la Umeme TANESCO jinsi ya kukabiliana na majanga ya Moto na taadhari za Umeme pamoja na kutoa elimu juu ya maboresho ya huduma za mawasiliano kwa Shirika la Umeme TANESCO na wateja kama vile njia ya Jisoti na kuahidi zoezi hili kuwa endelevu kwa maeneo yote ya Mkoa wa Kilimanjaro.





## HABARI KWA UFUPI

# TANESCO KINONDONI KUSINI WATOA ELIMU KWA WANANCHI HUDUMA YA JISOTI

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Kinondoni Kusini limeugana na wadau mbalimbali kukimbiza Mwenge wa Uhuru katika Wilaya ya Ubungo pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi ya njia mpya ya kutoa taarifa kupitia simu janja inayojulikana kwa jina la TANESCO JISOTI ambayo inampa fursa mteja kuwasiliana na mtoa huduma kupitia namba ya WhatApp **0748 550 000**.







## BODI YA WAHARIRI

1. Mha. Boniface Gissima Nyamo-Hanga - Mwenyekiti
2. Irene Gowelle - Mhariri Mkuu
3. Augustino Kasale - Mhariri
4. MayLoyceMpombo - Mwandishi
5. Shamu Lameck - Mwandishi
6. Charles Kombe - Mwandishi
7. Mwanaisha Mbita - Mwandishi
8. Prisca Kayaga - Mwandishi
9. Samia Chande - Mwandishi
10. Michael Sokotta - Mbunifu Kurasa
11. Ramadhani Shaibu - Mpiga Picha





TUFUATILIE KUPITIA

**KURASA ZETU ZA MITANDAO YA KIJAMII KUPATA TAARIFA SAHIHI ZA SHIRIKA**

www.tanesco.co.tz